Title: Alfred Jomo Sirleaf – THE BLACKBOARD JOURNALIST
Author: Stefanie Duckstein, HA Afrika/ Nahost
Editor: Susanne Fuchs
Translator: Tony Dunham
Sound Clips DALET: Learning by Ear: LbE_PEO_Liberia_Sirleaf_xxx

---

Characters:
Narrator: Female voice
Voice-over: Alfred Sirleaf, male, 35
Vox Pop, male, 25

---

**INTRO**

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kwa jina “Watu wanoleta Mabadiliko”, Mfululizo wa makala haya unakupa fursa ya kukutana na mashujaa wa kawaida katika maisha ya kila siku barani Afrika. Watu hawa ni jasiri, wakweli na wamejitolea. Wana mtazamo thabiti wa maisha ya usoni na wanaamini kuwa ndoto walizonazo watazifanikisha. Jiunge nasi katika safari inayotupeleka huko Monrovia, mji mkuu wa Liberia katika Afrika ya magharibi. Tunakutana na mwanahabari mwenye wazo kuhusu mbinu ya kuwafikishia watu habari.

1. *SFX: 24th Street*

Paji la uso wa Alfred Sirleaf limerowa jasho. Ni saa moja asubuhi na tayari joto limeanza kupamba kwenye mapaa ya bati katika jiji la Monrovia. Hata hivyo vifungo vya shati la Alfred vimefungwa mpaka juu na ameifunga tai yake barabara, kama inavyotakikana,

anafikiria Alfred, kwa sababu yeye ni mfanyabiashara. Alfred amesimama kwenye sehemu yake ya kufanyia kazi huku kelele za mtaa wa 24 zikiwa zimetanda kila upande, katika maeneo ya katikati mwa jiji la Monrovia.

2. *Sound Clip: Alfred (ENG)*

*"Kwa mshangao wangu mkubwa watu waliokuwa na mawazo kuhusu upashaji wa habari hawakufikia ndoto kama hii. 'Itawezekenaje, kuwa na gazeti barabarani? Ni sawa na kusema, Bwana Sirleaf – umechanganyikiwa au vipi ! Unawezaje kuweka gazeti barabarani ili watu wasome?' wote hao walikuwa na mawazo yanayofanana lakini hakuna hata mmoja wao aliyeweza kuona wazo hili."*

Wazo lake, linaloitwa, Daily Talk, yaani „Mazungumzo ya Kila Siku", ni gazeti la kila mtu, kwa wanaotembea kwa miguu, waendesha magari, na kila mtu. Ni gazeti lililo katika mfumo wa kibanda. Mbao tatu kubwa zimesimamishwa mbele ya kibanda hicho na kila siku asubuhi Alfred anatumia chaki kuandika taarifa za magazeti kwenye mbao hizo.

3. *SFX: Alfred talking to visitor*

Alfred Sirleaf anajiita mwandishi habari wa ubao. Yeye ni wa kwanza barani Afrika . Ni mtu machachari. Huwezi kuamini kuwa umri wake ni miaka 35. Anabadili sauti yake kila mara anapozungumza mara kwa sauti ya juu mara sauti ya chini, kwa sababu Alfred ana upendo mkubwa na kile anachokifanya. Ana

mipango kabambe kuhusu maisha yake. Mara nyingine anafikiri haraka kuliko anavyotamka, halafu anacheka.

4. *Sound Clip Alfred*

*"Ilikuwa Jumapili asubuhi tarehe 14 mwezi wa tano mwaka 2000, siku hiyo ndiyo niliyoanzisha shughuli yangu hii, hapa hapa."*

Kutoka wakati huo amekuwa akifika hapa kila siku asubuhi kabla ya pilikapilika kuanza. Kwa haraka, Alfred anaruka juu ya rafu na kufungua ofisi za gazeti la Daily Talk.

5. *Sound Clip: Alfred*

*"Kutoka hapa tunaingia sasa kwenye chumba cha habari. Ukiangalia hapa utaona haya maandishi makubwa CHUMBA CHA HABARI: USIINGIE BILA RUHUSA. OK. Hebu njoo hapa taratibu. OK. Sasa hapa tulipo ndio kwenye chumba cha habari."*

*FADE INTO:*

6. *SFX: Things being moved about (keep under narrator)*

Chumba kikuu cha habari. Sehemu ndogo inayomtosha mwenyewe. "Inama, la sivyo utajigonga kichwa chako!" anaonya Alfred huku akisogeza mabango yenye taarifa kuhusu askari watoto. Hapa anachuchumaa halafu kwa vidole vyake vilivyojaa chaki anaanza kuandika habari za siku hiyo. Kelele za barabarani na miale ya jua vyote vinapenya kupitia mianya iliyo kwenye ukuta wa mbao.

7. *Sound Clip: Alfred*

*"Chumba cha habari cha kawaida ni tafuti na hiki cha "Daily Talk" . Bila shaka unasikia kelele za magari yakipita. Kwa kawaida chumba cha habari huwa ni mahala patulivu. Hakuna kelele, kimepoa. Kila kitu kiko sawa. Lakini chumba cha Daily Talk hakiko hivyo. Chumba hiki cha habari kiko barabarani kwa sababu gazeti lililoandikwa kwa chaki ubaoni lipo hapa. Wakati naandika taarifa watu huwa wanapita na wengine wananigongea na kuniambia, Hey, wakati umefika, Daily Talk inafanya nini?"*

Alfred hahitaji umeme. Hahitaji kompyuta wala meza. Anachohitaji ni redio yake tu ya mkononi…

8. *SFX: Radio news, searching channel*

*"Oh, Taarifa ya habari inasomwa. … Ok, ninasikiliza taarifa mbalimbali . Wakati ninasikiliza… najaribu kutafuta ni taarifa zipi ninazofaa kuandika. … Zaidi natafuta redio za hapa hapa nchini. …ok, hii hapa ni stesheni moja ya hapa hapa"*

….brightly colored chalks….(Chaki zenye rangi kali)

9. *Sound Clip: Alfred*

*"… Halafu tuna rangi inayovutia zaidi kabisa ambayo ni ... Njano ya kuwaka. Rangi hii ya manjano hutumika kuandikia namba, wakati tunapozungumzia mamilioni ya dola. Au kwa mfano: Watu 6 wamehusika kwenye ajali ya barabarani. Rangi hii inatumika pia kuonyesha heshima. Kama tukizungumzia kuhusu rais wa Jamuhuri ya Liberia, au rais wa nchi yoyote ile, yaani watu mashuhuri."*

…Na la muhimu zaidi anawahitaji waandishi wake kutoka sehemu mbalimbali.

*10. Sound Clip: Alfred calls correspondent*
*“Nampigia simu mwandishi huyu sasa. Anaitwa Lucin de Ville. Yeye ni mwandishi wangu aliyeko katika jumba la Capital. Habari za asubuhi Lucin nakupigia kutoka “Daily Talk” Je kuna maendeleo gani? nakadhalika…...”*

Alfred ana zaidi ya wanahabari 200 kote nchini Liberia. Wanampasha habari na matukio yaliyo nje ya mji mkuu. Kwa mfano bei ya gesi inapanda kwa haraka katika eneo la Mashariki. Au kuhusu visa vya rushwa huko Kaskazini mwa nchi. Wakati mwingine waandishi hao huwa wanamtumia picha kwa kutumia simu zao za mkononi, halafu Alfred huzichapisha picha hizo kutoka kwenye mkahawa wa Internet ulio karibu na kisha kuzibandika pembeni ya taarifa zinazohusiana nazo.

*11. Sound Clip: Alfred*
*“Tunataka kuhakikisha kuwa kila mmoja anahusishwa. Kundi linalotutatiza zaidi ni kundi la watu ambao hawajui kusoma wala kuandika. Hakika tunataka watu hao pia wapate habari lakini je tutalitatua vipi swala hilo?”*

Anawafikia watu hao kwa njia ya kutumia maneno rahisi, picha na mifano.

*12. Sound Clip: Alfred*
*“Kwa mfano tukizungumzia kuhusu kofia ya samawati yaani walinda amani wa Umoja wa Mataifa , basi tunachora picha hiyo ya kofia ya bluu. Kwa hiyo mtu akipita na kuona mfano huo, atasema leo nimeona gazeti la “Daily Talk” limeandika kitu juu ya Umoja wa Mataifa.”*

Liberia bado inapata matatizo kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyotokea miaka 14 iliyopita. Kuna barabara chache tu zilizo na lami na umeme ni ule wa jenereta. Shirika la umoja wa mataifa la kutetea haki za watoto, UNICEF, linakisia kuwa kiwango

chini ya nusu ya raia wa Liberia wanaweza kusoma na kuandika. Takriban theluthi moja tu ya watoto ndio wanaokwenda shule. “Je watashiriki vipi katika ujenzi wa taifa lao, kwa mujibu wa historia yao?” Alfred anashangaa.

13. *Sound Clip: Alfred*

*“Akili iliyoerevuka ni akili iliyokamilika. Watu hawa wako gizani. Ni vipofu hawaoni mambo mengi yanayotokea. Hawajihusishi na yale yanayotendeka. Ndio maana nikaanzisha mpango huu. Ili niweze kuwafikia. Wengi wao hawajimudu hata kununua gazeti, hawana fedha za kununua jenereta wala televisheni, hawawezi kwenda kwenye mkahawa wa intaneti. Ni ghali sana. Umasikini, umasikini, umasikini. Nchi hii imezama kwenye umasikini hivi ninavyozungumza na nyinyi. Kuna haja kubwa ya kuwaelimisha watu. Hiyo ndio shida mojawapo kubwa inayotukabili. Lakini ukianza tu kuwapasha watu habari, kuwaelimisha, kuwafungua macho kutokana na yale ambayo yanatendeka, hakuna mtu atakayeweza kuwadanganya tena. Kuna watu ambao wana faida, wana uwezo, ambao nchi hii inahitaji. Ni lazima kuwafikia watu hao!”*

Zaidi ya miaka mitatu sasa Liberia inaongozwa na rais mwanamke bibi, Ellen Johnson-Sirleaf. Ni rais wa kwanza mwanamke barani Afrika. Jina la ukoo wa Alfred, ambalo ni Sirleaf, ni sawa na la rais huyo lakini hawana undugu.

14. *SFX: washing the blackboard, writing, spelling*

Huku Alfred aking’ang’ana kuandika habari mpya, wanaume wachache tayari wako nje wanasubiri ripoti yake kwa hamu kubwa.

15. *Sound Clip: VOXPOP, man*

*“Kila mara tunapopita, tunakuja hapa kupata habari karibu zote kwa kusoma gazeti hili. Na ninafikiri huwezi kupata habari kamili kutoka serikalini kwasababu serikali inatangaza mambo ya kujisifia*

*tu. Ni vyombo vya habari vya hapa nchini ndivyo vinavyotawanya habari kwa watu ili wapate kusikiliza taarifa kuhusu nchi yetu ya Liberia."*

Licha ya watu wengi kutaka kusoma taarisa anazozichapisha David, mara nyingi inakuwa vigumu kumfurahisha kila mtu.

16. *Sound Clip: Alfred*

*"Unajua shida tuliyonayo katika gazeti hili la "Daily Talk" ni kwamba unawasiliana na watu moja kwa moja. Yaani jinsi mtu anavyohisi. Kwa sababu namba yako ya simu inajulikana. Wanakuona. Mara nyingine unapokuwa ndani unaandika habari, wengine wanaingia, wengine hata wanakataa kukubali unachoandika. Wanabisha wanasema kuwa hawataki kile ninachokiandika. Lakini ukweli ni kwamba kila taarifa haiwezi kumfurahisha kila mtu. Haiwezekani. Huwezi kumfurahisha kila mtu."*

Ghafla bwana huyu muona mbali, ambae amejawa na ari na ndoto za siku za usoni anaingiwa na mawazo.

17. *SFX: Alfred's home*

Tunakwenda kumtembelea mke wake, Magrador, na watoto wake wawili wa kike. Alfred alitutaka tufanye hivyo. Ni muhimu sana kwake. Njia nyembamba iliyopinda inaelekea nyumbani kwake. Vyumba vidogo viwili vilivyojengwa kwa ukuta wa udongo na nyasi ndio nyumbani kwake Alfred. Watoto wanacheza nje kwenye mchanga.

18. *Sound Clip: Alfred*

*"Nina shida siwezi kumtimizia mke wangu mahitaji yake kwa sababu sina fedha. Sina kipato. Ni kwa nini nina endesha "Daily Talk" gazeti ambalo halinipi kipato? Nitaweza vipi kumiliki taasisi*

*ya mambo ya habari au shirika, Je nina ndoto isiyoleta kipato? Lakini ninaendelea kujitolea muda na nguvu zangu – Hakuna maana, bure kabisa, ninafanya upuuzi tu. Kwa sababu ya ndoto yangu ninazidi kupata shida na matatizo kwenye mahusiano yangu."*

Pesa za simu, pesa za teksi, na pia pesa za mkahawa wa intaneti – kinachotoka ni kingi lakini hakuna kinachoingia. Anaishi kwa misaada na kazi ndogo ndogo anazofanya hapa na pale. Juu ya yote hayo, hakuna kitakachomzuia kuendelea na "Daily Talk" anasema Alfred huku akiangalia pembeni.

*19. Sound Clip: Alfred*
*"Ninahisi kuwa watu wa Liberia wanahitaji msaada, kuna haja ya kuwasambazia habari. Kwa hivyo mimi sitavunjika moyo, sioni kama nitavunjika moyo kirahisi. Sidhani. Sifikirii."*

Halafu anaanza kuzungumzia juu ya wazo jipya, anazungumzia kuhusu maendeleo ya elektroniki ya "Daily Talk".

*20. Sound Clip: Alfred lang*
*"Mfumo wa kusambaza taarifa kutumia kipaza sauti haujakamilika bado. Tutaonyesha picha ubaoni. Ubao huo utabandikwa kwenye gari la matangazo. Si jambo la kawaida. Ni vigumu kidogo lakini hebu fikiria hebu piga picha hiyo mawazoni. Ngoja nieleze. Ni kama gari lililotengenezea na jukwaa…kama boya ..upande mmoja wa boya …"*

*(FADE INTO NARRATOR)*

Gari hilo litazunguka nchini kote, katika sehemu za mashambani. Litakuwa limejengewa ubao wa elektroniki nyuma wenye picha na taarifa za habari katika lugha zote mbalimbali nchini Liberia. Alfred, anasema mfumo huo utaanza kufanyika hivi karibuni.

**OUTRO**

Je umeipenda hadithi hii? Iwapo ungetaka kutuandikia maoni yako, au kusoma zaidi juu ya makala haya au labda pia ungetaka kusikiliza tena hadithi hii ya Alfred, tembelea kwenye mtandao wetu. Anuani yetu ni www.dw-world.de/lbe Asante kwa kusikiliza na ni matumaini yetu kuwa utajiunga nasi wakati mwingine kwenye hadithi nyingine mpya, katika makala haya ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kwa jina “Watu Wanaoleta Mabadiliko”. Hadi tutakapokutana tena. Kwaheri!

END